



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آتَيْنَا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَأْتِفُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَنْتُمْ تَخْلُقُونَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيَعْلَمُنَّ هُمْ دِيَمَهُ الَّذِي أَرَضَنِي فَمُّ وَكَبِدُوكُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْفِهِمْ أَمْ
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Taarifa kwa Vyombo nya Habari

Mauaji ya Shakahola: Ni Imani Pofu isokinaisha Akili

(Imetafsiriwa)

Polisi nchini Kenya wanaendelea na ufukuaji wa makaburi membamba kuitoa miili ya watu wanaoaminika kufaa njaa katika eneo la pwani ya nchi. Idadi ya vifo hadi sasa imefikia 89 huku miili zaidi ikitarajiwu kutolewa. Pasta Paul Mackenzie - mhubiri matata wa kanisa linalojulikana 'Good News International' lililoko katika la eneo la ekari 325 karibu na Mji wa Malindi, akiwataka wafiasi wake kukaa njaa kwa siku kadhaa wakiamini kufanya hivyo ni kuyapa mgongo maisha ya kidunia na ndio njia ya kwenda kukutana na Yesu.

Hizb ut Tahrir Kenya imeshtushwa na kitendo hiki cha kikatili na ingependa kuangazia yafuatayo:

Mauaji haya ya halaiki sio ya kwanza kufanyika kwa ulimwengu wa kikristo kwani historia yake kumesheheni visa kama hivi. Mwaka 2000, kulishuhudiwa mauaji ya Kanungu pale pasta mmoja wa Uganda kwa jina la Joseph Kibwetere alihusika na mauaji ya zaidi wakristo 900. Na mwaka wa 1978 kukashuhudiwa mauaji ya Jonestown huko Guyana ambapo kasisi Jim Jones aliwadanganya wafiasi wake waweze kujidunga sindano zenye sumu na mauaji mengi ya kutisha yaliyoegemea misimamo mibaya iliyotokamana na itikadi za kihamasa na maigizo pasi na kukinaisha akili ya mwanadamu.

Kiasili mfumo wa kirasilimali umemkosesha mwanadamu matumaini ambayo huchukua nafasi kubwa sana katika kumuongoza maishani, nayo hali hii kwa urahisi ikapatilizwa na makasisi ambao wengi wao huwadaa wafiasi wao wajitoe uhai kwa madai ya kuupata uzima wa milele kwani tayari wamekwisha kata tamaa maishani. Mfumo huu wa kirasilimali umeshindwa vibaya katika kusimamia mahusiano ya kijamii na kupelekeea utepetevu wa vyombo nya usalama, hali ngumu ya kiuchumi, hulka mbovu za kijamii na utawala fisadi wa Kidemokrasia hivyo kukatisha kabisa matumaini kwa jamii.

Kwa kuwa suala la imani lina unyeti mkubwa katika maisha ya mwanadamu, kwani ndio huunda mienendo yake kama mtu binafsi na kama sehemu ya jamii. Ni itikadi ndio inayompa mwanadamu fikra na fahamu zinazomfanya apate kuamka na kuendelea. Tunasema kwamba Uislamu ndio mfumo pekee ulio na itikadi yenye kuafikiana na maumbile ya mwanadamu na kumdhaminia utulivu, usalama, raha na matumaini hapa duniani na maisha ya Akhera. Katika mojawapo ya malengo ya Uislamu ni kulinda uhai na mali hivyo kitendo chochote kile kinachopelekeea kuondosha uhai wa mtu au mali kimekatazwa na kukashifiwa vikali na MwenyeziMungu pale aliposema:

(وَلَا تُنْفِوْ بِأَيْدِيْكُمْ إِلَى النَّهَلْكَةِ)

"Wala msijite kwa mikono yenu kwa maangamizo" [Al-Baqara 2:195]

Shabani Mwalimu

Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari wa Hizb ut Tahrir

Kenya